


**JIMBO KATOLIKI IRINGA**  
**TAASISI YA AFYA NA SAYANSI SHIRIKISHI TOSAMAGANGA (TIHAS)**



S.L.P 50 TOSAMAGANGA  
IRINGA

SIMU: 0769 432 532 (MKUU WA TAASISI) / 0762 482 704 (MHASIBU)  
BARUA PEPE: [tosamagangainstitute@gmail.com](mailto:tosamagangainstitute@gmail.com)  
TOVUTI: [www.tihas.ac.tz](http://www.tihas.ac.tz)

### **UTANGULIZI**

Tunashukuru kwa kuendelea kuwa mdau wa Elimu katika kada ya Afya kwa kupitia Taasisi yetu. Taasisi inakuarifu tarehe ya kufungua mwaka mpya wa masomo wa 2023/2024 kwa mkupuo wa mwezi wa tisa itakuwa ni tarehe **16/10/2023**. Taasisi yetu inatoa kozi mbili za afya ambazo ni Utabibu (Clinical Medicine) pamoja na Uuguzi na Ukunga (Nursing and Midwifery) kwa hatua ya Astashahada na Stashahada.

### **GHARAMA ZA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA (ORDINARY DIPLOMA IN NURSING AND MIDWIFERY) MWAKA WA PILI**

| Na | AWAMU  | ADA                | MALAZI (Hostel) |
|----|--|--------------------|-----------------|
| 1  | <b>Awamu ya kwanza</b> (Wakati wa kuripoti muhula wa kwanza) | 500,000            | BURE            |
| 2  | <b>Awamu ya pili</b> (01/01/2024)                            | 500,000            | BURE            |
| 3  | <b>Awamu ya tatu</b> (Wakati wa kuripoti muhula wa pili)     | 500,000            | BURE            |
| 4  | <b>Awamu ya nne</b> (01/07/2024)                             | 500,000            | BURE            |
|    | <b>JUMLA</b>   | <b>2,000,000/=</b> | BURE            |

**NB:**

1. Gharama za Ada iliyoinishwa kwenye jedwali ilipwe kwenye Kumbukumbu namba ya malipo (**Control Number**) ya mwanachuo kupitia Benki ya CRDB.
2. Ada haitabadilika katikati/ndani ya mwaka wa masomo, lakini inaweza kubadilika mwanzo wa mwaka wa masomo unaofuata kutegemeana na mabadiliko ya uchumi wa Taasisi, Jimbo na Nchi.
3. Ada unaweza kulipa yote au kwa awamu nne kama ilivyoainisha kwenye jedwali
4. Mwanafunzi asipotimiza kulipa ada kwa awamu husika hatapokelewa au atarudishwa nyumbani na akikaa nyumbani kwa muda wa siku 21 na zaidi atapaswa kurudia mwaka.
5. Wale tu ambao wamelipa nusu ya ada ya muhula ndio watakaosajiliwa kwenye muhula husika.
6. Ada ikishalipwa hairudishwi.

### **ADA YA MAZOEZI KWA VITENDO**

1. Wanafunzi watafanya mazoezi kwa vitendo katika jamii na kituo cha afya (Community field) katika moja ya maeneo yanayopatikana katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa vijijini kwa muda wa siku 28 kwa mwaka wa pili . Gharama za mazoezi kwa vitendo ni **Tsh. 200,000/=** mwanafunzi aje nayo mkononi wakati wa kuripoti muhula wa pili.

## MICHANGO MINGINE

1. Gharama ya mitihani ya Taifa ya Wizara ya Afya ni **Tshs.150, 000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti.
  2. Ada ya Udhibiti Ubora (Quality Assurance Fee) Tshs.**15,000/=** Kwa ajili ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundu na Mafunzo ya Ufundu Stadi (**NACTVET**), UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti.
  3. Matibabu Tshs.**52,400/=** kwa asiye na bima na kwa mwenye bima afike na bima yake (UJE NA FEDHA MKONONI)
  4. Mfuko wa serikali ya wanachuo ni **Tsh 10,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU Wakati wa kuripoti.
  5. Gharama za usajili kwenye Baraza la Uuuguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) **Tshs 30,000/=** UJE NA FEDHA TASILIMU wakati wa kuripoti kama hukulipa mwaka kwani huwa inalipwa mara moja tu kwa miaka yote mitatu ya masomo.
  6. Gharama za marudio ya mtihani (supplementary exam) ni **Tsh. 50,000/=** kwa somo (kwa atakae shindwa fikia wastani) na maombi ya mtihani maalumu (Special sit exam) ni **Tsh. 50,000** kwa kila somo ( kwa sababu maalum)

Tunakutakia maandalizi mema na KARIBU.

ASANTE

ERICK L. MSEMWA

Mkuu wa Taasisi

